TANGAZO LA SERIKALI NA. 189 la tarehe 21/3/2025

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 191)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 227(1))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 388 la 2024

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Dhamana ya Kuzingatia Masharti ya Mazingira za mwaka 2025 na zitasomwa kwa pamoja na Kanuni za Dhamana ya Kuzingatia Masharti ya Mazingira za mwaka 2024 ambazo katika Kanuni hizi zitajulikana kama "Kanuni kuu".

Marekeisho ya kanuni ya 11

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 11 kwa kufuta kanuni ndogo ya (3) na kuandika upya kama ifuatavyo:

"(3) Mkurugenzi wa Mazingira anaweza, kwa ombi la maandishi na kwa sababu za kutosha zilizotolewa na mwekezaji, kuongeza muda wa kuweka dhamana ya utendaji wa mazingira ambao hautazidi muda uliotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1)."

"(4) Mwekezaji ambaye atashindwa kuzingatia kanuni hii anatenda kosa, na akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu chini ya Sheria ."

Marekebisho ya kanuni ya 19

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 19-

(a) katika kanuni ndogo ya (2), kwa kuongeza maneno "si chini ya sita lakini si zaidi ya kumi na mbili" mara kabla ya neno "wajumbe"; na

(b) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (2) yafuatayo:

"(3) Kamati ya ufungaji wa mradi itakuwa kamati ya kusudi maalumu na itavunjwa baada ya kukamilika kwa ufungaji wa mradi ."

Marekebisho ya kanuni ya 22

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 22(3) kwa kufuta rejeleo la kanuni ndogo ya (3) na badala yake kurejelea kanuni ndogo ya (2).

Marekebisho ya Jedwali la pili

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali la Pili kwa kuongeza mara baada ya Muhtasari wa Sura inayohusiana na "Kifungu cha Fedha" yafuatayo:

"Tamko inajumuisha taarifa inayothibitisha ukweli au uhalisi wa maelezo yote yaliyotolewa katika Mpango wa Ufungaji ambao utakuwa na saini ya mwekezaji."

Dodoma,
19 Machi, 2025

HAMAD YUSUF MASAUNI
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira*